TANGAZO LA SERIKALI Na. 84 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 5(1))*

AMRI YA KUPANDISHA HADHI HALMASHAURI YA MJI WA GEITA YA MWAKA 2025

KWA KUWA, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa alitoa Notisi ya Kusudio la Kupandisha Hadhi Halmashauri ya Mji wa Geita kama ilivyoainishwa katika Notisi hiyo iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, Tangazo la Serikali Na. 819 la mwaka 2024;

NA KWA KUWA, baada ya muda wa Notisi kuisha, hakuna pingamizi au wasilisho lolote lililopokelewa na Waziri kuhusu kusudio la kupandisha hadhi Halmashauri ya Mji wa Geita.

HIVYO SASA, mimi MOHAMED OMARY MCHENGERWA, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa madaraka niliyopewa na kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, natoa Amri kama ifuatavyo:

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupandisha hadhi Halmashauri ya Mji wa Geita ya Mwaka 2025.

Tamko

**2**. Eneo la mamlaka ya halmashauri ya Mji wa Geita kama lilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Amri hii, linatangazwa kuwa mamlaka ya Mji chini ya mamlaka ya halmashauri ya Manispaa.

Jina la Halmashauri na nembo

**3**. Halmashauri ya Manispaa iliyotangazwa chini ya Amri hii itajulikana kama Halmashauri ya Manispaa ya Geita na itakuwa na nembo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii.

Muundo wa Halmashauri

**4**. Wajumbe wa Halmashauri ya Mji wa Geita watakuwa wajumbe wa Halmashauri ya Manispaa ya Geita.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2*)

MIPAKA YA ENEO LA MAMLAKA YA HALMASHASURI YA MANISPAA YA GEITA

"Kuanzia kwenye daraja lililopo kwenye Kinamasi cha Nyaruhwa, barabara ya Geita-Sengerema, mahali ambapo mipaka ya Wilaya ya Geita na Sengerema inakutana. Kisha kuelekea kwenye mwelekeo wa nyuzi 97 kwa umbali wa kilomita 0.529 hadi GV210. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 112 kwa umbali wa kilomita 2.610 hadi GV211. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 156 kwa umbali wa kilomita 5.283 hadi GV86. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 137 kwa umbali wa kilomita 3.735 hadi GV87. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 165 kwa umbali wa kilomita 3.275 hadi GV91, kwenye mdomo wa Mto Muhama. Kisha kufuata Mto Muhama hadi GV102. Kisha kuelekea Kusini Mashariki kufuata Mto Muhama hadi GV99. Kisha kuelekea Magharibi kufuata Mto Muhama hadi GV195A, kwenye barabara ya Bulela/Kaboha. Kisha kufuata Mto Muhama kuelekea Kaskazini Magharibi hadi GV194. Kisha kufuata Mto Muhama kuelekea Kaskazini Magharibi hadi GV193, kisha GV192. Kisha kuelekea Kaskazini kufuata Mto Muhama hadi GV185. Kisha kufuata Mto Muhama kuelekea Kaskazini Magharibi hadi GV186 kupitia GV189. Kisha kuelekea Kusini kufuata Mto Muhama katika mwelekeo wa nyuzi 189 kwa umbali wa kilomita 4.148 kupitia vilima vya Lugeye hadi GV230. Kisha kuelekea Kusini kufuata Mto Nyamugogwa hadi GV233 kupitia GV226. Kisha kufuata Mto Nyamugogwa kuelekea Kusini Magharibi kwa umbali wa kilomita 5.423 hadi GV227, kwenye Mto Lwamwizu Magharibi mwa Msitu wa Mienze. Kisha kufuata Mto Lwamwizu kuelekea Kaskazini Magharibi hadi GV64. Kisha kufuata Mto Lwamwizu hadi mdomo wake, kisha kuelekea Kaskazini Magharibi hadi GV231 kupitia GV218 kwenye barabara ya Mwagimagi/Bushishi. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 258 kwa umbali wa kilomita 2.268 hadi GV639, Kaskazini mwa Kijiji cha Msokole. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 296 kwa umbali wa kilomita 3.124 hadi GV701 kwenye Mto Nyalwanzaja. Kisha kufuata Mto Nyalwanzaja hadi GV383 kupitia GV377 na GV378. Kisha kuelekea Kaskazini kupitia vilima vya Ibsabageni hadi GV382. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 334 kwa umbali wa kilomita 2.358 hadi GV444. Kisha kuelekea Kaskazini Magharibi kufuata Bonde kati ya Vijiji vya Mkolani na Buyagu hadi GV445 kwenye barabara ya Buyagu/Mkolani. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 226 kwa umbali wa kilomita 6.182 hadi GV8. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 294 kwa umbali wa kilomita 1.00 hadi GV413 kwenye vilima vya Songambele. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 341 kwa umbali wa kilomita 0.654 hadi GV412. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 316 kwa umbali wa kilomita 1.280 hadi GV411. Kisha kufuata barabara ya Bufunda na Mpomvu kuelekea Kaskazini Magharibi kando ya Hifadhi ya Msitu wa Geita hadi GV417, Kaskazini Magharibi mwa vilima vya Samina. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 341 kwa umbali wa kilomita 5.202 kupitia Hifadhi ya Msitu wa Geita hadi GV425, Magharibi mwa Kijiji cha Nyakabale. Kisha kuelekea Kaskazini Magharibi hadi GV423 kupitia GV kwa umbali wa kilomita 3.3. Kisha kuelekea Kaskazini Magharibi kufuata Mto Komlale kupitia GV112, GV113 hadi GV114. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 90 kwa umbali wa kilomita 8.132 hadi GV111, kwenye makutano ya barabara ya Bugulula/Mtakuja. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 75 kwa umbali wa kilomita 3.595 hadi GV80A. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 313 kwa umbali wa kilomita 4.754 kupitia barabara ya Nzera hadi GV80. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 87 kwa umbali wa kilomita 5.637 hadi GV79. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 107 kwa umbali wa

kilomita 4.962 hadi GV94 katika Kijiji cha Kamhanga. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 124 kwa umbali wa kilomita 1.874 hadi GV2, kwenye Kilele cha Kanza. Kisha kwenye mwelekeo wa nyuzi 101 kwa umbali wa kilomita 2.085 kupitia barabara ya Kamhanga hadi GV97 kwenye Mto Komoyo. Kisha kuelekea Kaskazini Mashariki kufuata Mto Komoyo kupitia GV181, GV172 hadi makutano ya barabara ya Nyakaduha/Chabulong kwenye mdomo wa Mto Mkoba. Kisha kuelekea Kaskazini Magharibi kufuata Mto Mkoba kando ya mpaka wa Geita/Sengerema hadi daraja lililopo kwenye Kinamasi cha Nyaruhwa mahali pa kuanzia."

JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 3*)

NEMBO YA HALMASHAURI

Dodoma,
20 Disemba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*